PACEMAKER SERIES - 006

DARASA LA TANO
JARIBIO LA MTIHANI
KISWAHILI - LUGHA

2015

JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

1. Tumia penseli ya kawaida tu.

2. Hakikisha umeandika kwa karatasi ya majibu:-

(i) NAMBARI YAKO YA MTIHANI (ii) JINA LAKO (iii) JINA LA SHULE YAKO

3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika karatasi ya majibu na wala sio katika kijitabu cha maswali.

Muda: Saa 1 Dakika 40

Umepewa kifungu chenye mapengo kuanzia nambari 1 mpaka 15. Chagua jibu lifaalo kujazia nafasi zilizoachwa wazi.

Punda ni mnyama ___1___ ana faida ___2___ sana. Nyumbani ___3___ mnyama mwingine awa yupi anayefanya ___4___ kama punda. ___5___ ana uwezo wa kubeba mizigo ___6___ kama ___7___ . Vilevile huwa anafuata maagizo ana___8___pewa. Chakula ___9___ pia huwa si ___10___ . Huwa ni kidogo sana. Hivyo basi mkulima hawezi kutumia pesa nyingi . Tatizo moja___11___ ni kuwa akipandwa na ___12___ , huwa ___13___ hata anayemlisha. Ndio maana wahenga wakalinganisha mtu asiye na ___14___ na punda. Walisema methali "Asante ya punda ni ___15___ "

1.	A. ambae	B. ambayo	C. abaye	D. ambaye
2.	A. mingi	B. zingi	C. nyingi	D. jingi
3.	A. kuwa	B. hakuna	C. tuna	D. wana
4.	A. bidii	B. uzembe	C. ujinga	D. upuuzi
5.	A. wewe	B. wao	C. yeye	D. kwako
6.	A. zito	B. lizito	C. mizito	D. wazito
7.	A. pamba	B. shashi	C. nyembe	D. nanga
8.	A. zo	B. yo	C. lo	D. o
9.	A. anachokula	B. anazokula	C. anavyokula	D. analokula
10.	A. nyingi	B. kingi	C. vingi	D. wengi
11.	A. lake	B. yake	C. zake	D. wake
12.	A. furaha	B. hofu	C. huzuni	D. hasira
13.	A. anajua	B. anamjua	C. akijua	D. hamjui
14.	A. huzuni	B. taabu	C. fadhaa	D. shukrani
15.	A. ngumi	B. kofi	C. mateke	D. matumbo

Kuanzia swali nambari 16 mpaka 30, jibu kulingana na maagizo

16. Tegua kitendawili:

Mwanangu mvivu hapendi mlima

A. mto B. upepo

C. mzee D. gari

17. Andika kwa maneno: Vijiko 15

A. Vijiko kumi tano

B. vijiko kumi na vitano

C. Vijiko kumi na tano

D. Vijiko moja tano

18. Tumia kiashiria kujazia pengo

Kuta _____ zina nyufa nyingi.

A. nyingi B. zingineyo

C. hizi D. huu

19. Kanusha:

Baba yangu alisafiri jana.

A. Baba yangu hasafiri jana

B. Baba yangu hatasafiri jana

C. Baba yangu hakusafiri jana

D. Baba yangu hajasafiri jana.

20. Andika kwa wingi:

Godoro langu ni kubwa.

A. Magodoro yangu ni makubwa

B. Gqdoro yetu ni kubwa

C. Magodoro zenu ni makubwa

D. Magodoro yetu ni makubwa

21. Minyoo _____ ni hatari.

A. hawa B. huu

C. hii D. hizi

22. Tumia "ingine" kwa usahihi

Darasa _____ iina wanafunzi.

A. nyingine B. zingine

C. jingine D. mengine

23. Kitenzi ni gani katika sentensi hii?

Waliimba wimbo mzuri sana

A. Waliimba B. Wimbo

C. Mzuri D. Sana

24. Baba yangu ni mkali kama_____

A. nguruwe B. paka

C. simba D. ng'ombe

25. Akisami hii huitwaje $^{3}/_{4}$?

A. Theluthi nne B. Robo nne

C. Robo tatu D. Thuluthi mbili

26. Kinyume cha : Wachache

A. wakubwa B. wanene

C. wengi D. wazito

27. Sitakula miwa _____ sana.

A. mingi B. nyingi

C. kingi D. jingi

28. Chagua sentensi sahihi

A. Nala chakula kingi.

B. Kipepeo huu amekufa

C. Maria aligonjeka

D. Sipendi mambo nyingi

29. Kanga, bata, jogoo kwa jumla ni

A. kuku B. ndege

C. wadudu D. malaika

30. Rais anakaa kwenye

A. pori B. ikulu

C. mzinga D. rumande

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 - 40

Maria alikuwa mwanafunzi wa darasa la tano mwaka jana. Alipofanya mtihani wake wa muhula wa tatu aliweza kufanya vizuri sana. Kusema kweli alishikilia nambari ya kwanza katika darasa lao. Hata mwaka huu bado anaongoza katika darasa lake kwa kuwa hata katika mtihani waliofanya muhula wa kwanza, bado alishikilia nambari ya kwanza. Ni vigumu sana umpate Maria akipiga kelele darasani. Mwalimu anapofundisha yeye huwa **ametega masikio** yake ndi. Ni vigumu umpate Maria na utovu wowote wa nidhamu.

Hata hivyo marafiki zake ndio hupiga kelele darasani. Achieng, Kamau, Fatuma na Mutiso hupenda pia kuwasumbua wanafunzi wengine somo linapoendelea. Ni juzi tu Kamau alimrushia mwanafunzi mwenzake karatasi iliyotafunwa. Maria alipoona hivyo aliamua kutomsema mwenzake. Maria anastahili kujua kutosema makosa ni sawa na kukubaliana na makosa yenyewe. Hali hii pia humfanya aliyekosea kuendelea na makosa yayo hayo. Kwa mfano mara ya pili, Kamau alipokitupa kijijiwe kwa mwanafunzi mwenzake , alimkosa na badala yake kijijiwe hicho kikamgonga mwalimu.

Naye mwalimu bila kusita alimwadhibu Kamau papo hapo. Maria alipoona hivyo, alijilaumu kwa kutomsema Kamau mara ya kwanza. Hii ni kwa sababu, hangerusha kijijiwe hicho. Maria aliweza kuwashauri wenzake wasinyamaze wanapoona makosa. **Nao wanaofanya makosa wajue hawatafanya makosa hayo milele. Siku moja watashikwa.**

31. Mwaka huu Maria yuko katika darasa la
A. nne B. tano
C. sita D. saba

32. Katika mtihani aliofanya katika muhula wa tatu mwaka jana, Maria alikuwa nambari ngapi ?
A. Ya mwisho B. Ya pili
C. Ya kwanza D. Haijulikani

33. Ni vigumu sana umpate Maria
A. akilia
B. akiuliza maswali darasani
C. akisoma
D. akiongea darasani mwalimu anapofundisha

34. Ni nini maana ya **"kutega sikio"** ?
A. Kuongea B. Kusikiliza
C. Kuuliza maswali D. Kunyamaza

35. Mwanafunzi ambaye ana utovu wa nidhamu hana
A. adabu B. makosa
C. uhai D. amani

36. Ni nani hapendi kuwasumbua wanafunzi darasani ?
A. Achieng B. Kamau
C. Fatuma D. Maria

37. Makosa ya Maria ni kuwa
A. yeye ni mwerevu kuliko wenzake
B. yeye hupenda kusoma sana
C. yeye huficha wanafunzi wenye makosa
D. yeye hawasaidii wanafunzi katika mtihani

38. Usipomsema mwenye makosa
A. atakufanyia makosa hayo
B. atayaacha makosa hayo
D. ataanza kukusumbua
D. ataendelea na makosa hayo

39. Kamau alipomchapa mwalimu kwa kijijiwe,
A. alisamehewa B. aliadhibiwa
C. alifukuzwa D. alilaaniwa

40. Ni methali gani iliyo na maana sawa na taarifa iliyopigiwa mstari mwishoni mwa kifungu?
A. Kosa moja halimwachishi mke
B. Kosa ni kurudia kosa
C. Siku za mwizi ni arubaini
D. Asiyekujua hakuthamini

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41- 50

Mwanafunzi anapofanya mtihani , hastahili kupiga kelele hata na mwenzake. Iwapo unahitaji kitu chochote, jambo la maana ni **kuinua mkono** ili upate msaada wa mwalimu . Utashangaa wanafunzi wengine wakiendelea kuongea na wenzao utafikiria wako **gulioni** wakiuza bidhaa zao. Mtihani unastahili kuheshimiwa sana. Asiyeheshimu mtihani hupata alama za chini mno. Hii ni kwa sababu hata majibu anayoyaandika huwa hajali kama ni ya kweli au ya uongo. Yeye hutaka tu amalize amufurahishe mwalimu.

Wewe mwanafunzi wa darasa la tano, ningetaka uanze kuchukulia mtihani kama jambo la maana. Unapouheshimu mtihani, tabia hiyo itajengeka hata utakapokuwa katika darasa la nane. Mtihani wa K.C.P.E huwa na sheria kali sana. Iwapo hutaki kufeli katika mtihani huo wa K.C.P.E, basi anza leo kuheshimu mitihani mnayofanya darasani.

Tabia nyingine mbaya ni ile ya kuulizana maswali darasani. Wanafunzi wengine huwa hawajali kusoma ati ili waulize wakati wa mtihani. Wanapokaziwa na mwalimu hurudisha karatasi zao bila kujibu chochote. **Usipofuata mashauri haya utaathirika baadaye**.

41. Ufahamu huu unapinga
    A. kufanya mtihani
    B. kuuliza maswali
    C. kuzungumza
    D. kuongea wakati wa mtihani
42. ***Kuinua mkono*** ni sawa na
    A. kunyosha mkono juu
    B. kuona mkono
    C. kurusha mkono
    D. kupenda mkono
43. ***Gulioni*** ni wapi?
    A. Nyumbani B. Uwanjani
    C. Sokoni D. Garini
44. Anayeheshimu mtihani
    A. anapata alama za juu sana
    B. anapata alama za chini sana
    C. anafeli katika mtihani wake
    D. anachezea matokeo yake
45. Ukiheshimu mtihani
    A. utasahau na uanze kutojali
    B. utaendelea vivyo hivyo
    C. utafeli maswali mengine
    D. utamaliza haraka sana
46. Mwanafunzi wa darasa la nane hufanya mtihani gani?
    A. K.C.P.E B. wa kaunti
    C. wa wilaya D. wa tarafa
47. Haya yote ni ya kweli isipokuwa
    A. kuna wanafunzi wanaorudisha karatasi ya majibu bila kujibu.
    B. kuna wanafunzi wanaouliza wakati wa mtihani
    C. kuna wanafunzi wanaoongea maswali ya mtihani
    D. kuna wanaoongea na kupita vizuri sana
48. Mtihani unastahili
    A. kupuuzwa B. kuheshimiwa
    C. kuchukiwa D. kupendwa
49. Usipofuata mashauri haya utaathirika baadaye, ni sawa na kusema
    A. asiyesikia la mkuu huvunjika guu
    B. kidole kimoja hakivunji chawa
    C. Njia ya mwongo ni fupi
    D. adui mpende
50. Aya ya pili inamrejelea mwanafunzi wa darasa la
    A. 4 B. 5
    C. 6 D. 7